



Fati alikuwa msichana
mdogo, ambaye alikimbia
kama upepo, aliyependa
kucheka, na alijitahidi
kufanya yote aliyoambiwa



Siku moja, Fati walienda kwa baiskeli na baba yake shambani ili wakapalilie.



Ghafla, Fati alikuwa amechoka. Fati akasema, "Baba, kuna joto na nimechoka. Naweza kukaa chini ya mwembe?" Baba akasema, "Naam Fati, unaweza keti hapo. Ila, nakuomba usipande miti yoyote leo."



Fati aliketi chini ya
mwembe.



Fati alimchungulia baba yake. Alikuwa na kazi na hakumtazama. Kimya, Fati alianza kupanda mwembe.

Fati aliwaza, "Nitaketi kwenye tawi nzuri na kubwa. Ni mahali pazuri pa kupumzika na kula maembe mengi yaliyoiva." Aliketi na akala.



Baada ya kula maembe, Fati alishuka chini ...



Ilikuwa ni asali! Fati alipenda asali. Lakini hakuwapenda nyuki. Fati akatazama na kuona nyuki moja ndogo.

Fati aliwaza, "Kuna nyuki moja tu. Haitaniumiza nikipanda mti ili nitafute asali. "



Fati alimtazama baba yake.


Babake hakumtazama.

Kisha, Fati alipanda hadi juu
ya mti na kuchukua asali
kutoka shimo.



Fati aliwaza, "Nitaketi kwenye tawi hili nzuri, kubwa. Ni mahali pazuri kupumzika na kula asali nyingi yenyenye utamu. "

Aliketi na kulana kula.



Baada ya kula asali, Fati
alishuka.

Kisha akaona nyuki.

Wengi sana!

BZZZ! BZZZ! BZZZ!

Aliwakimbia nyuki.

Fati ran to her father.

Fati alimkimbilia baba yake.

Fati alikuwa akisonga na Fati alikuwa anahema.

Baba akasema, "Fati, umekuwa wapi?" Fati hakutaka kusema mahali alipokuwa.



Kisha akasema, "Angalia,
Baba, nina embe.

Ungependa kula? " Baba
akasema, "Hapana, asante
Fati.

Lazima tuende nyumbani
sasa. Mvua itanyesha"





Wakielekea nyumbani, Fati aliketi nyuma ya baba yake kwenye baiskeli. Mvua ilinyesha.



Baba alienda mwendo wa kasi kwa baiskeli.



Baiskeli iliangukia mguu wa Fati.





Nyumbani, mama na bibi waliulizia siku ilivyokua shambani.

"Jamani, maskini Fati,"
akasema bibi.

Lazima tuuangalie mguu
wako.

" Nao waliuangalia.

Na ikawa ndio mwisho wa
hilo.



